

**JINA LA MRADI:** Shughuli wezeshi kwa Serikali ya Tanzania kuridhia Marekebisho ya Kigali ya kupunguza matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa tabaka la hewa ya ozoni angani (*Enabling Activities for Kigali Amendment the Montreal Protocol on Phasing Down Hydrofluorocarbons*)

**MFADHILI WA MRADI:** UNEP

**LENGO LA MRADI:** Kuiwezesha Serikali ya Tanzania kutekeleza shughuli mbalimbali zitakazopelekea kuridhia Marekebisho ya Kigali yanayolenga kupunguza matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons.

**MUDA WA UTEKELEZAJI:** Januari 2019 - Januari, 2021

**GHARAMA ZA MRADI:** USD 85,000

#### **SHUGHULI ZINAZOTEKELEZWA CHINI YA MRADI**

- i. Kuendesha vikao kazi na wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa serikali kuridhia marekebisho ya Kigali yanayohusu kupunguza matumizi ya kemikali za hydrofluorocarbons (HFCs) ya Itifaki ya Montreal kuhusu kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni
- ii. Kuendesha semina za mafunzo kwa mafundi mchundo juu ya njia bora za kuhudumia majokofu na viyoyozi kwa kutumia kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HCFs) na mbadala wake;
- iii. Kufanya tathmini ya mfumo wa kisheria uliopo na kuendesha mkutano wa wadau mbalimbali kupitia taarifa ya tathmini ya kisheria kuhusiana na kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal ;
- iv. Kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mapendekezo ya serikali kuridhia marekebisho ya kigali yanayohusu kupunguza matumizi ya kemikali za hydrofluorocarbons (HFCs) ya Itifaki ya Montreal kuhusu kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni. Marekebisho haya yaliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo Septemba, 2019.
- v. Kutafsiri vifungu vya Marekebisho ya Kigali kwa lugha ya Taifa
- vi. Kuandaa na kusambaza vipeperushi mbalimbali ili kuelimisha umma kuhusu marekebisho ya Kigali;

- vii. Kutengeneza National Customs codes kwa kemikali jamii ya HFCs kwa kushirikiana na Mamlaka ya mapato Tanzania;
- viii. Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa sekta ya mafundi mchundo wanaohudumia majokofu na viyoyozi;
- ix. Kupitia upya Kanuni za Udhibiti wa Kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni pamoja na vifaa vinavyotumia kemikali hizo za Mwaka 2007 ili kujumuisha marekebisho ya Kigali